

**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Wednesday 22 May 2002 (morning)  
Mercredi 22 mai 2002 (matin)  
Miércoles 22 de mayo de 2002 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. Substantial references to a Part 2 work of the same genre are permissible but only in addition to the minimum of two Part 3 works. References to other works are permissible but must not form the main body of your answer.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Traiter un seul sujet de composition. La composition doit être basée sur au moins deux des œuvres étudiées dans la troisième partie du cours. La composition peut comporter des références importantes à une œuvre du même genre étudiée dans la seconde partie, mais uniquement en plus des deux œuvres de la troisième partie. Les références à d'autres œuvres sont permises mais ne doivent pas constituer l'essentiel de la réponse.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta debe basarse en al menos dos de las obras estudiadas para la Parte 3. Se podrán hacer referencias importantes a una obra de la Parte 2 del mismo género pero solamente como complemento a las dos obras de la Parte 3. Se permiten referencias a otras obras siempre que no formen la parte principal de la respuesta.

*Andika insha juu ya moja ya masuala yafwatayo. Jibu lako lazima liwe juu ya angalau kazi mbili za sehemu ya 3 ulizojitayarisha nazo. Lazima uingize katika jibu lako mjadala wa kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo mmoja kama inavyohusika. Majibu ambayo hayaegemei kwenye mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 hayatapata alama za juu.*

### **Tamthilia**

#### **1. Ama**

- (a) “Mara nyingi jina au anuwani ya tamthilia husimamia yale yanayojadiliwa ndani ya tamthilia yenyewe.” Je, unakubaliana na wazo hili? Linganisha vipi na kwa kiasi gani jina au anuwani za tamthilia mbili ulizosoma zinasimamia au kutosimamia maudhui yake.

*Au*

- (b) Jadili huku ukirejelea angalau kazi mbili ulizozisoma katika sehemu hii vipi waandishi wa tamthilia hizo wanayajadili matatizo ya jamii zao.

### **Riwaya**

#### **2. Ama**

- (a) Onyesha kwa kiasi gani waandishi wa kazi mbili za riwaya ulizozisoma katika sehemu hii wanavyotofautiana katika jinsi wanavyoimudu mbinu ya usimulizi.

*Au*

- (b) Jadili na kuonyesha kwa kiasi gani wahusika mviringo na kuaminika kwao ni vipengele muhimu katika kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

### **Ushairi**

#### **3. Ama**

- (a) “Sifa muhimu ya ushairi ni ile ya kujadili dhana au mada pana kwa maneno machache.” Katika angalau shairi moja ya kila mshairi katika kazi za washairi wawili ulizojitayarisha nazo, onyesha vipi sifa hii ya ushairi inavyofuatwa au isivyofuatwa na kwa taathira gani.

*Au*

- (b) Jadili upekee wa mtindo wa mshairi mmoja kulingana na mshairi mwengine wa kazi angalau mbili ulizozisoma katika sehemu hii.

## Riwaya ya Mapenzi

### 4. *Ama*

- (a) “Katika riwaya ya mapenzi waandishi huwanasa wasomaji wao baina ya lugha ya ramsia, raha za mapenzi na migogoro yake.” Kwa kutumia angalau kazi mbili ulizozisoma katika sehemu hii, onyesha kufanikiwa au kutofanikiwa kwa waandishi wa kazi hizo katika kutekeleza sifa hizi.

*Au*

- (b) Onyesha jinsi waandishi wawili wa riwaya ulizozisoma katika sehemu hii wanavyotofautiana katika kulikabili suala la mapenzi katika kazi zao na zingatia taathira za mbuni walizozitumia.

## Masuala ya Ujumla

### 5. *Ama*

- (a) “Mara nyingi katika kazi za fasihi wahusika wanawake wanatofautishwa sana na wahusika wanaume.” Linganisha jinsi waandishi wawili uliosoma kazi zao wanavyomtazama mwanamke katika kazi zao.

*Au*

- (b) Katika angalau kazi mbili ulizosoma, onyesha jinsi waandishi wake wanavyotofautiana katika matumizi ya lugha kisanaa.

*Au*

- (c) “Mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi, hasa katika baadhi ya tanzu, lazima awe ni msimulizi hodari.” Jadili huku ukitoa mifano ya kazi angalau mbili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (d) Kwa kutumia waandishi wawili wa kazi za fasihi ulizosoma, onyesha vipi wanayatumia mazingira katika kufanikisha sanaa na maudhui katika kazi zao.